# "ULEMAVU BARANI AFRIKA"
# EPISODE 5: " MASKINI HOHE HAHE"

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**List of characters / Episode 5:**

**MSIMULIZI**

**<u>SCENE ONE: TALK AFTER LUNCH IN THERESA'S HOUSE</u>**

- Theresa (mke, 65)
- Tofa (mke, 40)
- Zabibu(mke,15)

**<u>SCENE TWO : LAST LESSON IN SCHOOL</u>**

- Chitoto (mume, 18)
- Magoto (mume, 18)
- Karemi (mume, 18)

**<u>SCENE THREE: AT KAREMI'S DOORSTEP</u>**

- Theresa (mke, 65)
- Tofa (mke, 40)
- Oluanda (mume, 18)
- Zabibu (mke, 15)

**<u>SCENE FOUR: AT CHITOTO'S HOME BACKYARD</u>**

- Fagilio (mume, 42)
- Chitoto (mume, 18)

## SCENE FIVE: EVENING AT OLUANDA'S HOME

- Oluanda (mume, 18)
- Tofa (mke, 40)

### UTANGULIZI:

Nakusalimu na kukukaribisha tena,ikiwa ni awamu mpya ya kipindi chetu cha " **Noa bongo, jenga maisha yako** ". Hiki ni kipindi cha tano cha tamthilia hii inayomulika masaibu yanayowakumba ndugu wenzetu waliosahauliwa na kudharauliwa na jamii kwa isimu ya " **Ulemavu barani Afrika".** Taratibu kama tulivyoona katika kipindi kilichopita, Oluanda, ambaye kwa sasa ana ulemavu, anapigwa kumbo na jamii kiutangamano na kihekima. Hiyo ndiyo hali halisi kwa wengi wenye matatizo hayo barani Afrika. Je, atakubali kudidimizwa kabisa? Au atapigana jino kwa ukucha dhidi yake? Hebu tuyagundue haya katika kipindi hiki kinachoitwa " **Maskini hohe hahe**", kwanza kabisa tutabaruku na nyanya Theresa wakiwa mazungumzoni na Tofa baada ya chakula cha mchana.

## SCENE ONE: TALK AFTER LUNCH IN THERESA'S HOUSE

1. **SFX: CUTLERY BEING WASHED**

2. **TOFA:** (**Surprised)** Siamini ulionieleza! Theresa,unasema ati mume wako alikuwa kipofu? Na babako alikuwa na ngozi kama ya Zabibu? Pia yeye alikuwa zeruzeru? Uliweza vipi wewe kuyakabili hayo?

3. **THERESA:** Bora usadiki. Kwa hivyo nakuelewa vizuri unavyohisi Tofa. Unaona, baada ya kuishi na hao wawili, waliokuwa muhimu mno maishani mwangu, wote wakiwa na ulemavu fulani,nilijifunza kitu kimoja. Hata wakimbizi kutoka nchi jirani wanapewa hali nzuri kimaisha kuliko walemavu wa nchi hii.

4. **TOFA:** Huo ni ukweli, ukweli mtupu! Nilikuwa sijafikiria hivyo. Hebu mtazame binti yako Zabibu, mzaliwa wa papa hapa, lakini anachukuliwa kama mgeni na hawezi kuwa huru Abadan!

5. **THERESA:** Lakini hilo si kitu! La kusikitisha ni kuwa hawa watu, amabo wana uwezo wa kutenda makuu nchini, wamefanywa kuamini kuwa hawastahili kutangamana, bali sawa yao ni kuketi pembezoni mwa miji na kuomba omba **(emphatic)** hayo ni makosa hata kwa mwenye-

enzi Mungu!

6. **SFX:** **KNOCKING ON DOOR**

7. **ZABIBU:** **(Excited)** Nyanya niache nitazame ni nani anabisha…

8. **SFX :** **DOOR BEING OPENED**

9. **ZABIBU:** Ni Oluanda!

10. **MSIMULIZI:** Oluanda Aliiaga shule haraka baada ya mjadala na mwalimu wake mkuu Bi. Nina. Hakutaka kumueleza yeyote yaliomsibu ila mamake. Lakini kama shule ilivyo, mtu humweleza neno mwengine, naye akamdokeza mwengine, mwengine naye na mwengine.basi siku imalizikapo huwa kuna arafa tofauti tofauti zimeenea. Marafiki wa Oluanda wa zamani pia hawakujua ukweli ni upi.

**<u>SCENE TWO: LAST LESSON IN SCHOOL</u>**

11. **SFX: SCHOOL BELL RINGS, students chattering while leaving class**

12. **CHITOTO:** (**Excited)** Jamaa, Oya jamaa! Mumezisikia habari mpya?

13. **KAREMI:** Chitoto,sasa umezidi! Maisha ya Oluanda yamo ukingoni hivi sasa. Jitakase; muombe msamaha Oluanda pamoja na mamake.

14. **MAGOTO:** Ndio, twaweza kujaribu kusahau kuhusika kwako na ajali yake. Lakini Oluanda hayuko tena shuleni! La, hii si haki.

15. **CHITOTO:** Ngoja… Hebu subiri! Kwanza, sihusiki kamwe na ajali ya Oluanda.Alijileta mwenyewe, akaparaga mbuyu mwenyewe, na akaanguka mwenyewe, na pili, mimi sijamfukuza shule. Sasa jamaa, nimefanya makosa gani,eh?

16. **KAREMI:** Wewe chitoto ulimuacha peke yake alipoanguka vibaya na kuumia. Kumbe wewe muoga kama fisi?

17. **SFX :** **HARD SLAP ON FACE**

18. **CHITOTO:** Nyamaza Karemi! Hakuna mtu anasubutu kuniita mimi muoga! Mimi? Umesikia,hakuna!

19. **MSIMULIZI:** Hii ni fazaa kwa marafiki wa Chitoto ambao hawakutazamia haya, lakini je watanyamaza kuona mwenzao ananyanyaswa? Au watapaza vinywa vyao waseme ukweli?kwa sasa, tufulizie nyumbani kwa kina Karemi…..

**<u>SCENE THREE: AT KAREMI'S DOORSTEP</u>**

20. ATMO: OUTSIDE AMBIENCE

21. **TOFA:** **(Worried)** Oluanda, Mwanangu, kuna tatizo? Mbona umerudi mapema kutoka shule? Au

darasa lako…

22. **OLUANDA:** Hawanitaki tena shuleni mama.

23. **TOFA:** Una maanisha nini? Nani ? Kwanini?

24. **THERESA :** Tofa, mbona usimuache mtoto aingie ndani? Hujui kuwa kusimama kizingitini ni kufukuza wageni…

25. **ZABIBU:** **(sarcastic)** Wageni gani? huwa hatupati wageni sisi hapa nyumbani nyanya…

26. **TOFA:** La, Theresa. hatutaingia; acha anieleze papa hapa. Oluanda, kumetokea nini?

27. **OLUANDA:** Ni hivyo, Bila sababu. Lakini mwalimu mkuu aliniita afisini kwake, akanieleza kuwa ni kwa ajili ya manufaa yangu na ya shule nzima kwa ujumla kuwa niache kwenda shule ya watoto kamili, na uniorodheshe shule maalum.

28. **ZABIBU:** Karibu sana kilabu chetu!

29. **THERESA:** Zabibu! Hebu nyamaza, huyu msichana ana..anapenda mzaha mwingi. Sasa kajitayarishe uende shule ya ngumbaru.. jioni inakaribia.

30. **TOFA:** Ati umesema nini Oluanda? Umesema shule ya

watoto kamili? Una hakika hayo ndiyo maneno mwalimu aliyotumia?

31. **OLUANDA:** Ndio mama. Hivyo ndivyo Bi.Nina alivyoniambia. Tafadhali turudi nyumbani. Nataka kurudi nimalizie kutengeneza viatu vyako…

32. **TOFA:** **(raving mad)** Theresa,Unaweza kusadiki? Mtoto wangu sasa si mkamilifu? Hapana…sitakubali! Njoo Oluanda, nipe mkoba wako wa vitabu, twende nyumbani. Nashukuru kwa maongezi Theresa, tutaonana.

33. **THERESA:** Karibuni, Tofa, usihofu.. baada ya dhiki faraja!

34. **SFX:** **DOOR CLOSES.**

35. **MSIMULIZI:** Baada ya maongezi na Theresa, Tofa na kijana wake Oluanda pole pole walielekea mastakabuni mwao, kimya. Wakiwaza kimoyomoyo. Kumbe si mbali Fagilio atagunduwa siri kubwa kumuhusu Chitoto, ambayo kwake pia ilikuwa ni usiku wa kiza.

**<u>SCENE FOUR : AT CHITOTO'S HOME, IN BACKYARD</u>**

36. **SFX :** **OPENING OF BEER BOTTLE FOLLOWED BY GULPS; YARD AMBIENCE**

37. **CHITOTO:** **(Enjoying)** Mmmm… haya ndio maisha! Kila siku bia moja baada ya masomo. Natarajia babangu hatagunduwa…

38. **SFX:** **SUDDEN FOOTSTEPS RUSHING IN**

39. **FAGILIO:** Chitoto! Kumbe uko hapa? Nimekutafuta kote....

40. **SFX:** **BOTTLE SUDDENLY DROPPED ON GROUND**

41. **FAGILIO:** Hii ni nini? Eh Chitoto, ulikuwa unafanya nini na chupa ya pombe iliyoanguka?

42. **CHITOTO:** Si mimi baba… sio kitu.. tumetumwa shule tufanyie utafiti…

43. **FAGILIO:** **(cutting him short,annoyed)** Utafiti gani? Shule ipi? Njoo karibu.. Hebu songa karibu!

44. **SFX:** **SNIFFING IN AIR FOR BEER SMELL**

45. **FAGILIO:** **(Sarcastic)** Kwa hivyo hiyo shule yenu inawatuma mufanye utafiti wa kunywa pombe, sivyo? Hiyo ndiyo kemia inavyosomwa? Umekuwa ukinywa pombe tangu lini? **(Silence)**

46. **FAGILIO:** **(with emphasis)** Chitoto hukusikia nimekuuliza swali? Sitakuuliza tena mara mbili. Umekuwa

ukilewa kwa muda gani?

47. **MSIMULIZI:** Kama wahenga walivyohenga, mwana wa nyoka ni nyoka. Fagilio hakuamini kuwa tabia za mwanawe za kuanza kunywa pombe mapema zimekuja kumfagilia heshima chache aliyobakia nayo. Atapambana vipi na tabia hii? Adhabu ya tabia hii itakua nini? Usisahau Oluanda, aliyetimuliwa shuleni,anashuona viatu nyumbani. Na kwa mara yakwanza alimuhadithia ukweli mamake alipokuja kumtazama akishona viatu hivyo.

**SCENE FIVE: EVENING AT OLUANDA'S HOME**

| | | |
|---|---|---|
| 48. | **SFX:** | **POLISHING OF SHOES** |
| 49. | **TOFA:** | Shabash! Viatu vimerudi upya! Oluanda, sasa umekuwa stadi kweli. |
| 50. | **OLUANDA:** | Unasema kweli mama? Isiwe unanisifu tu kunipa moyo… |
| 51. | **TOFA:** | Hapana,sioni maana ya kukupaka mafuta kwa mgongo wa chupa. Kwangu uko sawa tena ushahitimu kabisa. |
| 52. | **OLUANDA:** | Kweli? Kwa sababu sina shida yeyote. Haya,viatu vyako vyote vya zamani nimevirekebisha. Viko humu mfukoni. |
| 53. | **SFX:** | **PLASTIC BAG CRUMPLING WHEN LIFTED** |

54. **TOFA:** Shukran mwanangu. Oluanda, mbona unajipa kazi hizi? Je ni vile ulivyonieleza awali? Kwamba hutoweza tena kuvaa viatu? **(sad tone)**

**55. OLUANDA: (Takes a deep breath then chuckles lightly)**

Kwani ni uongo mama? Maisha yangu yote sitohitaji tena viatu viwili bali kiatu kimoja. Lakini hiyo sio sababu. Nafanya hivi kwa sababu…. **( hesitates)**

56. **TOFA:** Kwa sababu gani? Nieleze . usinifiche mimi ni mamako...

57. **OLUANDA:** Nahofia mama. Nimewatazama wote walio kama mimi na walio na ulemavu kama mimi hapa Maganye, walio vipofu, mabubu, viziwi na wengineo.Nikaona wote hali yao ni moja. Wote ni maskini hohehahe. Sitaki kuishia fukara.

58. **TOFA:** Oluanda, mwanangu. Niko na wewe. Kwanini uhofie sasa?

59. **OLUANDA:** Kwa sababu mimi ni mmoja wao mama. Ndio. Leo niko na wewe, nashukuru sana Mungu kwa hilo. Lakini tunajuaje kesho utakapokuwa….sitaki hata kutamka maneno hayo.. nitabaki peke yangu. Sina marafiki, sina familia, sina elimu, sina tumaini. Nawaelewa

jinsi wanavyopata dhiki.

60. **TOFA:** Oluanda, mwanangu. Kwa hivyo hukuona ajira nyengine ila ya kushona viatu?

61. **OLUANDA:** Haijalishi iwapo nitapata pesa.. sitaomba mtu! Hilo ndilo laniogopesha,

62. **TOFA:** **(Stressing)** Imekwenda wapi ndoto yako ya kuwa muhandisi, utakayejenga barabara ya kwanza ya lami hapa Maganye? imekwendapi ndoto hiyo?

63. **OLUANDA:** Mama niliiavya ndoto hiyo siku ile nilipoanguka kutoka kwenye mbuyu. Ya nini tufiche mama, umewahi kumuona muhandisi yeyote mwenye kwenda kwa magongo?

64. **TOFA:** Ni kweli,sijaona kitu kama hicho, lakini huoni hii ni kama changamoto… ningependa wewe uwe muhandisi wa kwanza kutembea kwa magongo hapa Maganye.

**HITIMISHO:**

Nasaha iliyopewa mwana na mamake. Mwana ambaye kesha funga milango ya fanaka kwa ajili ya ulemavu. Je, oluanda atayafuata?au atayapuuza na afuate ajira duni kama wengine? Je, Chitoto yuko tayari kutubia? Bado kuna mengi yatakayokujia kupitia tamthilia hii “ **Ulemavu barani Afrika”.** Kusikiliza tena kipindi hiki au chengine tembelea tovuti

zetu www.dw-world.de/lbe. usisite kutupa maoni yako au hisia zako. Mpaka wakati wa kipindi kijacho. Nakutakia maisha mwanana.